Biashara ya Viumbe wa Porini walio Adimu, wakati wa kufanya biashara za nje na mazao yote ya utumiaji.

Tanzania inakusudia kuendelea kubakiza idadi yake ya tembo wa Afrika iliyo katika Jedwali la I ya Makubaliano hayo, kwa siku za usoni. Hata hivyo Tanzania itaendelea kukaribisha jitihada za mataifa mengine yenye mbuga, kuhifadhi tembo wao, mradi tu jitihada hizo zifanyike kwa kuzingatia Makubaliano na pia kwa namna ambayo Tanzania inaamini kwamba haitasababisha uwindaji haramu zaidi wa tembo wa Afrika, ndani ya mipaka yake.

Waziri atazingatia na kuimarisha vizuri muhimu wa sheria na kanuni zinazotakiwa kutekeleza ulinzi na uendeshaji wa shughuli za tembo.



MPANGO WA USIMAMIAJI WA TEMBO WA AFRIKA  
*Loxodonta africana* (Blumenbach) NCHINI TANZANIA

1. UTANGULIZI

Sera ya Tanzania kuhusu tembo wa Afrika inatambua kwamba tembo ndiye aina moja kuu na ya kipekee kwa utajiri wa urithi wa asili kwa Tanzania. Mnamo miaka ya 1970 ilikisiwa kwamba Tanzania ilikuwa na idadi ya tembo kiasi cha 365,000 na hivi leo idadi hii imepunguzwa hadi kufikia kiasi cha 50,000. Kadhalika eneo la mbuga ya tembo nchini Tanzania limepungua kutoka karibu asilimia 90 ya nchi mnamo miaka ya 1950 hadi kufikia karibu asilimia 50 hivi leo. Kupotea huku kwa kiasi cha idadi na eneo la mbuga kumetokana hasa na uwindaji haramu wa tembo kwa ajili ya meno yao na pili kwa sababu ya kupotea kwa makazi ya tembo kulikotokana na kuongezeka kwa idadi ya watu. Upoteaji wa utajiri huu wa urithi wa asili na raslimali hii inayoweza kuzalishwa upya pamoja na uvutiaji huu wa kitalii ni janga. Hata hivyo ingawa sera ya Tanzania inatambua kwamba idadi yake ya tembo inapaswa kurejeshwa, Tanzania haikusudii idadi yake ya tembo irejee kufikia kiasi ilivyokuwa mnamo miaka ya 1970 kwa kuwa, bila shaka, idadi hiyo itaongeza idadi ya migogoro iliyopo baina ya tembo na binadamu, ukizingatia idadi ya watu inayoongezeka. Badala yake, mpango wa uendeshaji unataka uifikie katika maeneo mbalimbali yanayolindwa, na una matumaini makubwa kwamba makundi ya tembo yanaweza yakaendelea kuishi katika maeneo yaliyokaliwa kwa halali na binadamu kwa kuimarisha sera zinazosisitiza uhifadhi uliojengwa katika ridhaa ya jumuiya. Kwa kuwa Tanzania ndiyo iliyokuwa mpendekezaji mkuu wa orodha ya Jedwali la I inayohusu tembo wa Afrika kwa mujibu wa Makubaliano ya Kimataifa ya Kudhibiti Biashara ya Viumbe wa Porini walio Adimu (Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora, yataitwa CITES) mnamo mwaka 1989 na kwa kuwa idadi ya tembo wa Tanzania bado inahitaji muda ipate kurejea, Tanzania itaendelea kuunga mkono uorodheshaji wa Jedwali la I kuhusu idadi yake ya tembo wa Afrika kwa upande wa meno ya tembo kwa siku za usoni zijazo. Hata hivyo Tanzania inakusudia kutafuta njia za kuongeza thamani ya kichumi ya tembo wake, hasa kwa manufaa ya jumuiya za maeneo wanamoishi, kadri mipaka ilivyowekwa na uorodheshaji wa Jedwali la I. Kwa hiyo, mpango huu wa uendeshaji unakusudia kuhimiza:

- a) urejeshaji wa idadi ya tembo wa Tanzania na uendeshaji wake kwa misingi ya kisayansi;
- b) ulinzi kamili wa tembo wa Tanzania katika maeneo yanayolindwa yaliyochaguliwa na utumiaji wake kwa njia ya Utalii na utazamaji wa wanyamapori;
- c) utumiaji wa tembo uliodhibitiwa kwa kuzingatia uwindaji wa burudani ulio na mipaka katika maeneo yanayolindwa pale panapofaa;
- d) upunguzaji wa maingiliano kati ya tembo na binadamu katika maeneo yaliyokaliwa kwa halali na binadamu kwa kuimarisha sera zinazosisitiza mipango ya uhifadhi uliojengwa kwa ridhaa ya jumuiya, na pia pale inapowezekana, kwa kudhibiti wanyama wenye matatizo.



## 2. SHERIA

Kwa mujibu wa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na 12 ya 1974 (itaitwa Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori), tembo anaweza akawindwa au kutumiwa kwa leseni iliyotolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori (ataitwa Mkurugenzi). Tembo wenye meno yenye uzito unaopungua kilo 12 kwa jozi wanaeleweka kama ni Wanyama wa Taifa kwa mujibu wa Amri ya Kuhifadhi Wanyamapori (Wanyama wa Taifa) ya 1974. Kwa hiyo, hakuna mtu isipokuwa na kwa mujibu wa kibali cha maandishi cha Mkurugenzi kilichotolewa mapema, atakayewinda, au, teka au zingira tembo yeyote aliye na meno yasiyo na uzito huu. Sababu ya pekee ya kuvunja amri hiyo ni kwamba tembo wanaweza kuuliwa kwa lengo la kulinda maisha ya binadamu na mali.

Hakuna utumiaji kwa ajili ya chakula utakaoweza kufanyika katika Hifadhi za Taifa kwa mujibu wa Sheria za Hifadhi za Taifa, CAP. 412 ya 1959. Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro CAP. 413 ya 1960, Mamlaka yaweza kuamuru kuzuia kuondoa mimea na wanyama, au watu kubeba au kutumia silaha, nyavu au sumu ndani ya Hifadhi.

Upigaji marufuku wa kufanya biashara ya meno za tembo ndani ya nchi umekuwa ukitekelezwa kwa miaka mingi. Ipo adhabu kwa kufanya biashara ya meno ya tembo kwa mujibu wa Sheria ya Kuhujumu Uchumi na Njama Na. 13 ya 1984. Tembo wa Afrika aliorodheshwa kwenye Jedwali la I ya CITES mnamo 1989. Kwa mujibu wa Kifungu cha III cha CITES, hairuhusiwi kufanya biashara ya Kimataifa kwa kutumia tembo, sehemu yake yeyote ya mwili au chochote kitokanacho na mwili wake kwa malengo ambayo kimsingi ni malengo ya biashara.

## 3. UNDESHAJI KATIKA MAENEO YANAYOLINDWA

- i) Katika Hifadhi za Taifa na ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, tembo watalindwa kikamilifu na mazingira yataendeshwa ili kukuza tangu urejeaji wa idadi yao na muundo wa marika yao hadi idadi kwa eneo inayotakiwa kwa kila makazi. Utumiaji wa tembo wa Tanzania katika Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro litatengwa maalum kwa ajili ya watalii kuona wanyama.
- ii) Katika Hifadhi zote za Akiba, tembo watalindwa kikamilifu na mazingira yataendeshwa ili kukuza tangu urejeaji wa idadi yao na muundo wa marika yao hadi idadi kwa eneo inayotakiwa kwa kila makazi. Utumiaji wa tembo wa Tanzania katika Hifadhi za Akiba utakuwa ni pamoja na uwindaji wa burudani wenye mpaka na kwa ajili ya watalii kuona wanyama.
- iii) Ndani ya maeneo yaliyo wazi au yale ambamo wanyama hudhibitiwa, ulinzi na urejeaji wa tembo utahimizwa. Hata hivyo, tembo walio katika maeneo ya aina hii ndio changamoto dhidi ya shughuli za uendeshaji wao kutokana na migogoro iliyopo baina yao na shughuli halali za binadamu



ya maeneo haya. Zaidi ya haya hayumkini migogoro hii itazidi kuongezeka katika siku za mbele kwa sababu tatu. Kwanza, kadri idadi ya tembo itakavyokuwa ikiongezeka, pili, kutokana na kwamba tembo watakuwa hawatiwi misukosuko na majangili tena na hivyo kutawanyika katika maeneo ya jirani yasiyokaliwa na watu yanayolindwa na tatu, kadri idadi ya watu inavyoongezeka. Njia za utumiaji zitafutwa ambazo husisitiza manufaa ya kiuchumi ya tembo na aina nyingine za wanyamapori wakaa katika maeneo haya kwa watu wa maeneo hayo, na kwa kufanya hivyo kuongeza uvumilivu wao na kuwakubali tembo ambao hukaa kati yao. Njia hizo zitakuwa ni pamoja na, pale zitakapofaa, utazamaji wa wanyama wa kitalii, uwindaji wa burudani wa kipimo kwa wanyama mafahali wenye kimo cha kukidhi haja ya kupata nyara, au uuzaji kwa watalii wawindaji wale wanyama wanaostahili kuuliwa ili kuhifadhi maisha ya watu na mali, pamoja na sera zinazosisitiza uhifadhi wenye misingi ya ridhaa ya jumua zinazohusu aina nyingine za wanyamapori. Mgao wa mapato ya kiuchumi, uliotokana na makubaliano, kutokana na matumizi ya aina hii utatolewa kwa ajili ya jumua zinazokaa katika maeneo hayo.

#### 4. UREJEAJI WA IDADI

Mojawapo kati ya migogoro ya aina kubwa mbili kati ya tembo na binadamu iliyokuwepo Tanzania katika miaka ya hivi karibuni imekuwa ni uwindaji haramu wa tembo, hasa kwa ajili ya meno yao. Mgogoro huu umepelekea athari kuu mbili kwenye idadi ya tembo wa Tanzania, kwanza kwa kusababisha upunguzaji mkubwa wa idadi na pili kwa kubadilisha miundo ya marika na jinsia ya makundi yaliyobaki. Mabadiliko katika miundo ya rika na jinsia yamejitokeza kwa namna mbili kuu. Kwanza, idadi kubwa ya tembo wakubwa imeuliwa kwa kuwa walikuwa na meno makubwa na hivyo tembo mbuguma wenye umri wa zaidi ya miaka 40 na tembo mafahali wachache wenye zaidi ya miaka 20 ndio waliobaki. Pili kuna kizazi cha tembo vijana kilichopotea katika miaka ya uwindaji mzito wa haramu kutokana ama na kiwango cha kuzaliwa idadi ndogo ya tembo au kiwango kikubwa cha vifo vya ndama wakati wa kipindi hicho. Hivyo basi urejeaji wa tembo wa Tanzania unahitaji uongezekaji wa idadi na pia kurudi kwa muundo wa kawaida wa rika na jinsia.

Idadi ya tembo wa Tanzania imeshuka kutoka karibu wanyama 365,000 katika miaka ya 1970. Hata hivyo Tanzania imeamua kuweka lengo la idadi ndogo kuliko hiyo kwa ajili ya urejeaji wa idadi yake ya tembo. Uchaguzi huu umefikiwa ili kupunguza migogoro kati ya tembo na binadamu, kwa kuzingatia ukweli kwamba sehemu kubwa ya eneo la mbuga za tembo huingiliana na maeneo ambayo yamekaliwa na watu kwa halali na pia kwamba idadi ya watu nchini Tanzania inazidi kukua. Kwa sasa eneo la mbuga za tembo lipo katika maeneo makuu au maeneo mfumo shirika saba ambayo ni eneo, mfumo shirika la Serengeti, eneo mfumo shirika la Kilimanjaro-Amboseli, Mkomazi katika eneo mfumo shirika la Tsavo, eneo mfumo shirika la Tarangire-Manyara, eneo mfumo shirika la Selous, eneo mfumo shirika la Ruaha na eneo mfumo shirika la miombo magharibi pamoja na maeneo ya mbuga ndogo za Saadani na Rumanyika-Ibanda (Tarakimu Na 1). Kwa kuzingatia ukubwa wa mbuga za maeneo, hivi sasa Tanzania imejiweka kiwango cha mwisho cha urejeaji kuwa kiasi



cha tembo 120,000 (Orodha Na 1). Tarakimu hii imetokana na kuzidisha tarakimu mbili. Kwanza ni makadirio yaliyo sahihi ambayo yameweza kupatikana kutokana na taarifa za kitaalamu zinazohusu idadi kwa eneo kwa upande wa tembo ambayo inaweza kupatikana katika makazi mbalimbali yenye kupata viwango mbalimbali vya mvua lakini bila kusababisha kuchuja kwa eneo hilo. Makadirio ya aina hii ndiyo huitwa 'Idadi kwa eneo mwafaka kwa uendeshaji'. Pili ukubwa wa Hifadhi za Taifa, Hifadhi za Akiba na Eneo la Hifadhi yaliyo katika maeneo ya mbuga kwa sasa. Kipimo hiki cha mpaka wa kiwango cha juu hapana shaka nighafi kwa kuwa, kama kilivyo, kutokana na makadirio ambayo si sahihi sana ya idadi kwa eneo na pia kwa kutoyahusisha makadirio ya idadi ya tembo ambao wangeweza kuwa nje ya maeneo yanayolindwa yasiyokaliwa na watu. Kwa hiyo kwa sasa kiwango hiki cha mpaka wa juu ni cha lengo la muda tu kwa ajili ya urejeaji ambacho chaweza kurekebishwa kadiri ushahidi zaidi unavyopatikana.

Malengo kwa ajili ya urejeaji wa miundo inayotakiwa ya rika na jinsia kwa ajili ya tembo wa Tanzania ni magumu zaidi kuyaeleza na kuyapima kuli' o malengo ya kupata idadi ya tembo. Katika maeneo yanayolindwa yasiyokaliwa na watu, Tanzania inakusudia kuruhusu makundi ya tembo kuongezeka hadi kufikia kiwango ambacho watakuwa wamepata mtawanyo imara wa marika na makadirio ya uwiano wa jinsia wa asilimia 40 ya mafahali na asilimia 60 ya majike baina ya tembo wenye umri zaidi ya miaka 15.

#### 5. USHIRIKISHWAJI WA JUMUIA KATIKA KUHIFADHI TEMBO

Kumekuwa na mgogoro mkuu wa aina ya pili kati ya tembo na binadamu katika miaka ya karibuni nchini Tanzania ambao umesababisha kupotea kwa mbuga za tembo nje ya maeneo yanayolindwa yasiyokaliwa na watu. Hii imetokana na ushirikishaji wa masuala yafananayo ya hali, pamoja na uharibifu wa mazingira wa binadamu na uharibifu wa maisha ya binadamu na mali unaofanywa na tembo, hasa mazao yao, jambo ambalo matokeo yake huwa ni kuwauwa tembo. Ulinzi wa maisha ya binadamu na mali yake, umekuwa, na unaendelea kuwa, sababu ya uuaji wa dharura wa tembo wengi kwa ajili ya hifadhi ya mazao, wanaokisiwa kuwa kati ya wanyama 500-1000 kila mwaka. Ingawaje shughuli hii huwapa wanajumuiya wa maeneo fidia ya nyara ni yenye madhara sana ya kupoteza manufaa mengine yatokanayo na yenye thamini kamili kiuchumi kwa tembo aliyeuliwa. Matokeo yake tembo wengi zaidi huuliwa katika maeneo yale kuliko ambavyo ingelazimu au ingefaa. Kwa kutumia mipango mizuri ya hifadhi yenye ridhaa ya jumuiya, Tanzania itajaribu kuongeza thamani ya tembo ambao italazimu wauliwe ili kulinda mazao na kuimarisha katika jumuiya za maeneo hayo thamani ya wanyamapori kwa jumla na kuongeza uvumilivu kwa wanajumuiya kuhusu tembo. Kwa kutumia maeneo ya utafiti wa majaribio karibu na Hifadhi za Akiba ya Selous, itaamuliwa mgao upi wa idadi ya tembo watakunwa badala ya uuaji wa dharura wa tembo kwa kulinda mazao, na sehemu ya idadi hiyo itatolewa kwa watalii wawindaji, pamoja na sehemu ya mapato na nyama yote itakayopatikana kurudishwa kwa jumuiya za maeneo hayo. Lakini hata hivyo kwa wanyama watakaouliwa wenye meno yenye uzito chini ya kiwango cha chini cha uzito, mwindaji hataruhusiwa kusafirisha meno hayo nchi za nje. Ufanisi wa umbali kidogo wa kiasi cha kilomita 50, wa uzio wa umeme pia utajaribiwa ndani ya eneo, hasa lile lenye migogoro mingi kati ya binadamu na tembo katika eneo la utafiti wa majaribio la Selous.



## 6. UTUMIAJI

Utumiaji wa tembo kwa ajili ya watalii kuona wanyama katika Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, na maeneo yenye Hifadhi za Akiba utahimizwa. Vitengo vinavyofanya tembo waendeleo kukaa katika hali yao ya asili na kutowasababishia bughudha kutoka kwa watalii au vifaa vya watalii vitahimizwa.

Tanzania inaamini kwamba tasnia iliyopangiliwa vema kwa ajili ya uwindaji wa burudani itachangia sana kupunguza uwindaji haramu na uuaji haramu wa tembo katika jitihada za kulinda maisha ya binadamu na mali. Hivyo basi utumiaji wa tembo kwa ajili ya uwindaji wa kitalii ulio na mpaka ndani ya Hifadhi za Akiba utaruhusiwa pale ambapo ufuatiliaji umeonyesha ya kwamba miundo ya marika na jinsia unaruhusu uwindaji huo. Tanzania itahakikisha kwamba idadi yake ya tembo haitumiki kwa ajili ya wawindaji wa burudani na kuambulia hasara ya upungufu wa wanyamapori (Azimio la Kongamano wa CITES 2.11). Lengo hili litapatikana kwa njia mbili. Kwanza, wawindaji watalii, tangu msimu wa kuwinda wa 1991 wameruhusiwa kuwinda tu tembo mafahali wenye meno zenye uzito wa zaidi ya kilo 25 kila jino au yenye urefu wa mita 1.75 kila jino, kipimo ambacho ni kikubwa cha kutosha kuliko kile kilichokuwa kimewekwa awali na Sheria ya Kuhifadhi ya Wanyamapori. Pili kwa kuzingatia ukaguzi wa daima kuhusu idadi ya wanyama na kiwango cha nyara na idadi ya wanyama wanaouliwa na wawindaji watalii kutatolewa uamuzi iwapo kiwango kilichopo kitafaa kwa uwindaji au la. Usafirishaji nje wa nyara za tembo utafanywa kwa mujibu wa CITES na Sheria ya Kuhifadhi ya Wanyamapori.

## 7. UTEKELEZAJI WA SHERIA NA AKIBA YA MENO YA TEMBO

Tanzania haitasamehe hata kidogo uwindaji haramu wa tembo. Mamlaka zinazohusika katika ngazi mbalimbali za maeneo yanayolindwa na yale yasiyolindwa mathalani Shirika la Hifadhi za Taifa (itaitwa TANAPA), Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (itaitwa NCAA) na Idara ya Wanyamapori, zitafanya kila jitihada kuongeza uwezo wake wa utekelezaji wa sheria ili kupata kiwango kikubwa cha kuwang'amua wote wenye moyo wa uhalifu katika mbuga na pia kuendeleza na kuhifadhi kumbukumbu za taarifa za upelelezi wa wahalifu waliotangulia wajulikanao. Tanzania itapiga hatua ya kuzileta pamoja na kuzilinganisha kumbukumbu zake za upelelezi, kuharakisha ubadilishanaji wa taarifa kati ya mamlaka za kitaifa na za kimataifa. Tanzania inaunga mkono kwa dhati Makubaliano ya Lusaka ambayo yanalenga kukuza ushirikiano mkubwa zaidi wa kikanda katika utekelezaji wa sheria. Zaidi ya hayo, adhabu zitakazotolewa za uuzaji haramu wa tembo kwa ajili ya meno au nyama zitazidishwa pale itakapofaa, ili kuonyesha dhati ubaya wa kosa hili.

Tanzania hairuhusu biashara ya meno ya tembo nchini wala katika kiwango cha Kimataifa kwa sababu ya upigaji marufuku biashara hiyo nchini na pia kufuatana na uorodheshaji wa Jedwali Na. I ya CITES. Kujihusisha na biashara ya meno ya tembo kunachukuliwa kama kosa kubwa sana. Ushirikiano kamili wa kiwango chochote cha gharama utatolewa kwa serikali yoyote au mamlaka ya polisi, iwe ya kitaifa au ya kimataifa, unaokusudia kupeleleza vitendo au watu wanaotuhumiwa kuendesha vitendo



hivyo, viwe vinahusu meno yatokanayo na tembo wa Tanzania au tembo kutoka nchi nyingine inayopitia Tanzania.

Tanzania inakusudia kuendelea kutunza akiba yake ya meno ya tembo mahali pa usalama na kuiongeza akiba hiyo kutokana na utafishaji wa meno ya haramu yatakayotokea siku za usoni. Meno yote katika akiba hii sasa yanapimwa uzito, kuwekwa alama za kudumu na kuandikishwa katika daftari la kumbukumbu kwa kazi hii itaendelea kufanywa kwa ajili ya nyongeza yoyote itakayoletwa baadaye. Kumbukumbu za nyongeza zitakazoletwa baadaye zitatenganishwa kufuatana na kule yatokako iwe kutokana na uwindaji halali, vifo vya kawaida na wanyama wenye madhara ama utafishaji wa zile za uwindaji haramu. Tanzania pia itashiriki katika uundaji wa taarifa unaofanywa na taasisi ya Kimataifa ya "TRAFFIC International" ili kuwa na benki ya taarifa ya Kimataifa ya akiba ya meno ya tembo. Kwa kujua kwamba biashara yenye msingi wa biashara ya meno kwa sasa ni jambo lisiloweza kufanyika, uwezekano wenye manufaa utatafutwa ili kuipa akiba ya Tanzania thamani ya kiuchumi kwa namna kwamba masharti ya CITES hayatafunjwa, kwamba rundo lililopo halitaharibiwa kwa kuchomwa moto au uharibifu mwingine, kwamba meno hayo hayataingizwa katika soko haramu na kwamba pesa zitakazotokana na shughuli hii zitatumika kwa shughuli zinazohusiana sana na uhifadhi wa tembo.

#### 8. MAJUKUMU YA KIMATAIFA

Majukumu ya Kimataifa ya Tanzania kuhusu CITES na kujihusisha katika biashara ya meno yamekwishaelezwa na uungaji mkono wa Tanzania kuhusu Makubaliano ya Lusaka umekwishatolewa. Tanzania itajihusisha katika jitihada nyingine za Kimataifa kuhusu uhifadhi wa tembo ndani na nje ya mipaka yake. Kwa siku za karibuni Tanzania haikusudii kujiunga na kituo cha Kusini mwa Afrika cha Soko la Meno ya tembo (hapa kitaitwa SACIM). Hata hivyo Tanzania, kwa kutumia uanachama wake katika Jumuiya ya kiuchumi ya SADC kuhimiza kwa vitendo zile nchi zilizojiunga na SACIM kufanya kila njia kuhakikisha kwamba meno ya tembo hayapiti SACIM mpaka kwanza yajulikane kwa uhakika kule yalikutoka na pia kwamba biashara hiyo inayofanywa haisababishi kuwepo uwindaji haramu wa tembo katika nchi nyingine zenye hifadhi za tembo. Mara, na iwapo, masharti haya yatatekelezwa Tanzania itaunga mkono wanachama wenzake wa SADC katika umoja wa SACIM.

Tanzania itaendeleza pia ushirikiano na majirani zake kuhakikisha kuwa kuna urejeaji wa idadi na hadhi ya tembo wanaovuka mipaka ya mataifa kama vile katika maeneo yafuatayo: Kati ya Hifadhi ya Akiba ya Mkomazi na Tsavo nchini Kenya; kati ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na Amboseli nchini Kenya; katika eneo mfumo shirika la Serengeti ambalo sehemu yake kubwa iko Tanzania na sehemu nyingine nchini Kenya; karibu na Ras ya Senga iliyo mpakani mwa Tanzania na Uganda; kati ya Hifadhi za Akiba za Rumanika na Ibanda nchini Tanzania na ile ya Akagera nchini Rwanda; na kati ya eneo la Mwambesi lililo Kusini mwa Tanzania na Kaskazini mwa Msumbiji. Kwa upande wa tembo katika maeneo mfumo shirika ya Tsavo na Serengeti ambayo yamo katika maeneo yanayolindwa na yanachangia mipaka ya Kimataifa, lengo hili laweza kutimizwa kwa kutumia jitihada za utekelezaji wa sheria ulioimarishwa ndani ya maeneo yanayolindwa. Changamoto ya pekee inaletwa na tembo wa eneo la Kilimanjaro na Amboseli, kutokana na idadi kubwa ya binadamu linalozunguka Hifadhi



za Akiba kwenye eneo la Kilimanjaro. Lengo la kuendelea kuwa na upenu hadi kwenye mpaka wa kimataifa utaimarishwa kwa kiwango fulani na upanuzaji unaotarajiwa wa Hifadhi za Taifa ya Kilimanjaro na utengenezaji wa upenu wa tembo wa Kilimanjaro na kwa upande mwingine lengo hilo litatimizwa kutokana na upanuzaji wa shughuli kuzunguka eneo hili. Lengo la kuwepo upenu hadi Msumbiji linaimarishwa na kazi ya uhifadhi uliojengwa katika ushirikishwaji wa jumua ambayo inafanyika hadi Hifadhi za Akiba ya Selous. Itlazimu hivi karibuni kuanzishwa utafiti wa kujua mambo muhimu ya kufanya ili kuhifadhi tembo karibu na mpaka wa Rwanda.

## 9. UFUATILIAJI NA UTAFITI

Tanzania ina mahitaji kipaumbele sita ya ufuatiliaji na utafiti kuhusu jitihada zake za kuhifadhi makundi ya tembo wake, mathalani kuhusiana na utawanyaji na ukubwa wa idadi; muundo wa marika na jinsia, nyendo katika majira na ukubwa wa mbuga za tembo katika maeneo yanayolindwa sehemu za magharibi mwa Tanzania, ufuatiliaji wa mafanikio ya jitihada za utekelezaji wa sheria na kiwango cha migogoro kati ya tembo na binadamu na uendeshaji wa urekebishaji wa uwindaji wa burudani wa idadi iliyopimwa. Undani wa haya mahitaji kipaumbele sita ni kama ifuatavyo:

- a) Upimaji kutoka angani wa makundi makuu yote ya tembo utafanywa katika vipindi vya kila miaka miwili au mitatu ili kufuatilia mabadiliko ya idadi, mtawanyiko na urejeaji kuhusu idadi. Mbinu za upimaji wa ardhini pia zitazidi kuimarishwa ambazo huwahusisha ama wanasayansi au wafanyakazi wa nyika katika kutekeleza wajibu wao wakati wa doria za kutekeleza sheria ili kujua mabadiliko ya idadi na mtawanyiko.
- b) Mbinu za upimaji wa ardhini zitatumiwa pia na wafanyakazi wajuzi kujua uwiano wa jinsia na umri katika makundi muhimu hasa katika maeneo mfumo shirika ya Greater Ruaha, Selous na Tarangire, ili kufuatilia urejeaji wa mfumo wa marika na jinsia wa tembo. Katika Hifadhi za Akiba kama vile Selous na Rungwa-Kizigo, utafiti kama huu utatumika pia kujua upatikanaji wa mafahali ya kimo cha kutoa nyara.
- c) Kuna taarifa chache sana kuhusu nyendo wakati wa majira na ukubwa wa mbuga za tembo waishio ndani au kati ya maeneo yanayolindwa yaliyoko Magharibi mwa Tanzania. Ni muhimu kujua kiwango ambacho tembo hutembea kati na ndani ya Hifadhi za Taifa ya Katavi "lililopendekezwa kuwa" Hifadhi za Akiba ya Rukwa, eneo mfumo shirika la Greater Ruaha, Hifadhi za Akiba ya Ugalla na Hifadhi za Akiba ya Moyowosi ili kuweza kufuatilia urejeaji wao na kujua njia za uendeshaji ili kupunguza kabisa migogoro baina ya tembo na binadamu na kuanzisha utumiaji wenye manufaa.
- d) Sharti kuu la kufanikisha uhifadhi wa tembo ni kujua mafanikio ya jitihada za utekelezaji wa sheria dhidi ya uwindaji haramu. Vipaumbele vinategemea uongezekaji wa utaalamu wa ufuatiliaji kwa wafanyakazi wa nyika wanapotimiza wajibu wao wa kutekeleza sheria na pia kwa uanzishwaji wa ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za upelelezi



kuhusu wahalifu wajulikanao na pia kesi zinazohusu ufanyaji biashara ya meno ya tembo.

- e) Kiwango cha utatuzi au uongezekaji wa migogoro baina ya tembo na binadamu kinahitaji ufuatiliaji wa makini. Huu upatikanaji kwa ukusanyaji wa taarifa za nchi nzima kuhusu idadi ya tembo waliouliwa na kujeruhiwa kwa kuvamia mazao na idadi ya watu waliojeruhiwa au kufa, kwa kutumia utafiti wa kiwango cha uharibifu wa mazao katika sehemu kadhaa muhimu za maeneo yaliyofanyiwa utafiti na kwa kuona mafanikio ya majaribio yoyote ya kutumia uzio wa umeme, hasa karibu na Hifadhi za Akiba ya Selous, na kwa kufuatilia mafanikio ya miradi yote ya uhifadhi unaoshirikisha jumua kuhusu mawazo ya wenyeji wa maeneo yanayohusika juu ya wanyamapori kwa jumla na tembo kwa pekee.
- f) Ufuatiliaji na uwekaji wa viwango vya utumiaji wa manufaa wa makundi ya tembo kwa ajili ya kupata nyara kutokana na uwindaji wa burudani utafanikiwa hasa kwa upimaji wa ukubwa wa nyara na idadi ya tembo waliouliwa katika kila eneo, na pia kutokana na taarifa za mabadiliko katika ukubwa wa idadi na muundo wa rika na jinsia.

Mapendekezo zaidi kuhusu miradi ya utafiti isiyotumika sana kuhusu maumbile ya tembo itafikiriwa na mamlaka ya Wanyamapori yanayohusika mathalani TANAPA, NCAA na Idara ya Wanyamapori, kutegemea aina ya eneo linalolindwa ambapo utafiti umependekezwa, na Taasisi ya Utafiti ya Wanyamapori ya Serengeti.

#### 10. UREKEBISHWAJI WA MPANGO

Mpango utarekebishwa na kuanishwa na wakati, itakapolazimu, na Mkurugenzi na utawasilishwa kwa Waziri kila miaka mitatu kwa ajili ya idhini.

Mpango huu umetayarishwa kwa hisani ya Mradi wa Mpango na Tathmini ya Usimamiaji Wanyamapori, umegharamiwa na USAID na kusimamiwa na AWF na WWF.



Table 1: Approximate preferred management densities and total numbers of elephants to which Tanzania wishes its population to recover.

Orodha Na 1: Makisio ya idadi kwa eneo ya uendeshaji unaotakiwa na jumla ya tembo ambao Tanzania ingependa ipate urejeaji wa idadi hiyo.

Ecosystem	Preferred density per sq km	Protected Area	Size in sq km	Desired upper population
Eneo mfumo wa shirika	Idadi kwa eneo itakiwayo kwa kila km ya eneo mraba	Eneo linalolindwa	Ukubwa wa eneo kwa km za eneo mraba	Kiwango cha juu cha idadi inayotakiwa
Serengeti	0.25	Serengeti NP	15,500	3,900
		Ngorongoro CA	9,000	2,200
		Maswa GR	2,200	600
Kilimanjaro	0.25	Kilimanjaro NP&GR	1,600	400
Tsavo-Mkomazi	0.75	Mkomazi GR	3,400	2,500
Tarangire-Manyara	0.75 1.5	Tarangire NP	2,600	2,000
		Lake Manyara NP	330	500
Selous	1.0	Selous GR	55,000	55,000
		Mikumi NP	3,230	3,200
Greater Ruaha	1.0	Ruaha NP	12,950	13,000
		Rungwa-Kizigo-Muhesi GR	15,500	15,500
Western Miombo	0.5	Katavi-Rukwa	12,500	6,000
		Ugalla GR	5,000	2,500
		Moyowosi-Kigosi GR	20,100	10,000
Approximate upper numbers	Idadi ya juu inayokisiwa			120,000






Figure 1: Approximate range of the elephant and preferred management densities in different protected areas within the main ecosystems in Tanzania, based on Table 1.

Tarakimu Na 1: Idadi ya juu ya tembo kwa eneo nchini Tanzania Orodha Na 1.